
# LONDA

## RWANDA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE



# RIPOTI YA 2020

PARADIGM INITIATIVE

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ

# LONDA

## RWANDA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Imechapishwa na Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Jean-Pierre Afadhali
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



# LONDA

**RWANDA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Rwanda, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Rwanda. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri .

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

## YALIYOMO


UTANGULIZI 1

TASNIA YA TEHAMA NA SERA 2

UKIUKAJI WA UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI NA COVID-19 3

FARAGHA NA UFUATILIAJI 4

UFIKIAJI NA GHARAMA YA MTANDAO NA TEKNOLOJIA 5

JINSIA NA UFIKIAJI 6

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 7



Rwanda ni nchi ndogo inayozungkwa na nchi kavu iliyopo Afrika Mashariki na yenye idadi ya watu takriban milioni 12.6, kulingana na Taasisi ya Takwimu ya Kitaifa ya Rwanda.[1] Mji mkuu Kigali unakua kila uchao na huduma za kisasa za teknolojia na ongezeko la uhamiaji mjini limebadili hali ya jiji kwa miongo miwili iliyopita.

UTANGULIZI

# HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA RWANDA

Mji mkuu ni kitovu cha utawala na uchumi. Mwaka huu janga la COVID-19 limekwamisha maeneo kadha ya shughuli za nchi hiyo ikiwa ni pamoja na haki za kidijitali, uchumi na afya ya umma kw vile serikali ilipambana na virusi hivyo hatari kwa kuanzisha hatua kadha za kuzuia mkurupuko huo.

**COVID-19**
***iliathiri haki za dijiti, uchumi na afya ya umma***

Nchi hiyo inabainiwa kuwa mojawapo wa nchi yenye utulivu wa kisiasa na uchumi unaokua kwa kasi na yenye mabadiliko ya kijamii na kiuchumi barani Afrika. Serikali ya Rwanda inayoongozwa na Rais Paul Kagame imejizolea sifa tosha ulimwenguni na msaada wa kifedha kutoka kwa wafadhili na taasisi za kifedha za kimataifa katika miongo miwili iliyopita kwa mfano wake wa maendeleo.[2] Tangu mauaji ya kimbari ya 1994, ambapo watu wapatao 800,000 walipoteza maisha kulingana na Umoja wa Mataifa, mazingira ya kisiasa yametawaliwa na chama tawala cha Rwandan Patriotic Front (RPF) na vyama vingine vidogo shiriki vya kisiasa katika kile kinachojulikana kama Jukwaa la Ushauri la Kitaifa la Mashirika ya Kisiasa.[3]

Rais Kagame ameshinda chaguzi tatu mnamo 2003, 2010 na 2017. Bwana Kagame anasifiwa mara nyingi kwa kuigeuza nchi hii ya Afrika mashariki kuwa mfano bora wa maendeleo.

1. National Institute of Statistics of Rwanda: November 2020, http://www.statistics.gov.rw/
2. The Loyalty of Keeping Rwandans abroad in Check: BBC News Africa: 19 November 2020, https://www.bbc.com/news/world-africa-54801979
3. National Consultative Forum of Political Organization, http://forumfp.org.rw/index.php?id=42

Walakini, mtindo wake wa uongozi mara nyingi hukosolewa na mashirika ya haki za binadamu na upinzani kuhusu rekodi mbaya ya haki za binadamu, kuwanyamazisha wakosoaji, vyombo vya habari na asasi dhaifu ya kiraia.[4]

## TASNIA YA TEHAMA NA SERA

Wizara ya TEHAMA na Ubunifu wa Rwanda inaratibu sera na mipango inayohusiana na TEHAMA ikifuatiwa na mamlaka ya udhibiti, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Rwanda (RURA). RURA iliundwa na Sheria nambari 39/2001 ya 13 Septemba 2001 na dhamira ya kudhibiti huduma fulani za umma pamoja na mitandao ya mawasiliano na / au huduma za mawasiliano, miongoni mwa nyinginezo. Sheria hii ilirekebishwa zaidi na kubadilishwa na Sheria Nambari 09/2013 ya tarehe 01/03/2013,[5] ikiipa RURA jukumu la kudhibiti mawasiliano ya simu, teknolojia ya habari, utangazaji na teknolojia zinginezo za kielektroniki, ikiwa ni pamoja na mtandao na habari nyingine yoyote ya sauti na video na teknolojia ya mawasiliano. Kwa kuongezea, Mamlaka ya Jamii ya Habari ya Rwanda, shirika tanzu la Wizara ya TEHAMA husaidia serikali katika masuala ya kuifanya Rwanda kuwa ya Kidijitali.[6]

Sekta ya mawasiliano nchini Rwanda ina waendeshaji wawili wa mtandao wa rununu, watoa huduma 24 wa mtandao (ISPs), muuzaji mmoja wa jumla wa 4G na mtoa huduma ya mtandao, watoa huduma wawili wa vituo, na muuzaji mmoja wa jumal hadi kufikia Septemba 2020. Waendeshaji wakuu wa mawasiliano ya simu ni MTN-Rwanda na Airtel.[7] Telecom Liquid, zamani ikijulikana kama Rwandatel, hutoa huduma ya ASP na huduma zingine za mtandao kama vile broadband ya nyumbani. Upenyaji wa mtandao ni 62,9% hadi kufikia Machi 2020, kulingana na takwimu kutoka kwa mdhibiti wa mawasiliano.[8] Walakini, umudu wa vifaa na ufikiaji mdogo wa broadband unapanua pengo la kidijitali. Takwimu zinaonyesha 37% ya nyumba hazimiliki simu, wakati 74.3% ya wasajili wa rununu hutegemea zaidi 2G au huduma za polepole za mtandao wa 3G.[9]

Mnamo 2000 Rwanda ilizindua 'Ruwaza 2020' mpango wa maendeleo wa serikali kuafikia hadhi ya uchumi unayotegemea maarifa na uchumi ya kati ifikapo 2020. Mipango ya Miundombinu ya Habari na Mawasiliano (NICI) (2000 - 2015) ilipitishwa kuongoza programu za TEHAMA zilizounganishwa na Ruwaza 2020. Ufikiaji wa mtandao wa rununu wa nchi ni wa juu wa 93.5% kwa 3G wakati ufikiaji 4G ni wa 96.6% hadi kufikia Januari 2020.[10] Mkonga wa mtandao (Fiber optic) unakadiriwa kufikia zaidi ya kilomita 3,300 kulingana na mtandao wa Korea Telecom Rwanda.[11] Licha ya hili, matumizi halisi ya broadband yangali ya chini kulingana na idadi ya wasajili walioripotiwa na waendeshaji mtandao wa rununu.[12] Wakati upenyaji wa mtandao unaongezeka kwa 62,3% hadi kufikia Juni 2020, upenyaji wa 4G bado uko chini kwa 5.1% kulingana na data kutoka kwa mdhibiti.[13] 74% kwa sasa wanategemea 2G yenye huduma chache, ambayo ni ujumbe mfupi wa simu (sms) na

4. Rwanda Country Profile, BBC News: 17 September 2018, https://www.bbc.com/news/world-africa-14093238
5. Rwanda's official Gazette, 2013, https://rura.rw/fileadmin/docs/report/Official_Gazette_no_14_bis_of_08_04_2013.pdf
6. Rwanda Information Society Authority,2017, https://www.risa.rw/home/
7. Report for Licensed ICT operators,2020, https://rura.rw/fileadmin/Documents/ICT/statistics/Report_for__Licensed_ICT_Operators_as_of_Septemebr_2020.pdf
8. Report of Internet subscriptions per category, 2020, https://rura.rw/index.php?id=164
9. Accelerating Digital Transformation in Rwanda,2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda
10. Accelerating Digital Transformation in Rwanda,2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda
11. Korea Telecom Rwanda, 2020, https://www.ktrn.rw/about
12. Accelerating Digital Transformation in Rwanda, World Bank, 2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda
13. ICT and Telecom statistics, 2020, https://www.rura.rw/fileadmin/Documents/ICT/statistics/ICT_and_Telecom_Statistics_report_as_of_June_2020.pdf

sauti, kulingana na Benki ya Dunia.[14] Kuanzia Septemba 2020, kiwango cha jumla cha umeme kinachowezesha uunganishaji na ufikiaji kilikuwa 56.7% ya nyumba. Nchi inatarajia kuunganisha 100% ya nyumba ifikiapo 2024 wakati watumiaji wenye tija wataunganishwa kufikia 2022, kulingana na wakala wa nishati ya umma.[15]

Vituo vya huduma ya mtanda (Telecentres) pia vimesaidia raia kufikia huduma za kidijitali haswa maeneo ya vijijini.[16] Mwisho wa mipango ya tatu ya NICI mnamo 2015, nchi hiyo ilipitisha Mpango Kabambe wa Smart Rwanda 2020 kuendeleza ajenda ya mabadiliko ya kidijitali nchini hadi 2020 na zaidi.[17] Licha ya mafanikio ya miundombinu, haki za kidijitali na ujumuishaji bado ni ndoto kwa wengi wakati pengo la jinsia linapozi kupanuka ikiwemo mapungufu mengine ya kidijitali. Mnamo mwaka wa 2020, COVID-19 ilidororeshsha hali hiyo kwenye mambo kadha ikiwa ni pamoja na faragha, uhuru wa kujieleza mtandaoni, ufuatiliaji, utambulisho wa kidijitali, ufikiaji.[18]

## UKIUKAJI WA UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI NA COVID-19

Watayarishaji wa maudhui mtandaoni wanaoshiriki maudhui kwenye YouTube, na mpiga picha walikamatwa kwa madai ya kupuuza kanuni za COVID-19. Mnamo 2018, nchi ilitunga Sheria Nambari 60/2018 ya 22/8/2018 kuhusu kuzuia na kuadhibu ya makosa ya uhalifu wa mtandaoni. Sheria hiyo inakosolewa kwa kutumia ugaidi na usalama wa kitaifa kama sababu ya baadhi ya vifungu vyake vya ukandamizaji.[19] Hatua kadhaa zilizuia uhuru wa kujieleza mtandaoni maana wanablogi kadha, Mnamo Julai 13, 2020, mpiga picha Reuben Hamuli alikamatwa kwa madai ya "kuchapisha na kueneza uvumi mtandaoni".[20] Kulingana na polisi, mwanamume huyo alitumia ukurasa wake wa Twitter kutoa madai ya "uongo" kwamba alikamatwa kimakosa. Kifungu cha 39 cha Sheria Nº 60/2018 kuhusu Kinga na Adhabu ya Makosa ya Mtandaoni kilinukuliwa katika kesi hii.[21] Sheria inaadhibu kuchapishwa kwa uvumi na mara nyingi hutumiwa kuminya uhuru wa kusema.

Mnamo Aprili 2020, watendaji kadhaa wa vyombo vya habari walikamatwa kwa madai ya kukiuka kanuni za COVID-19.[22] Wakiwemo Théoneste Nsengimana, mkurugenzi wa Umubavu TV, kituo cha Runinga cha mtandaoni. Kwa kuongezea, Dieudonné ambaye anaendesha Ishema TV, idhaa

> ***Mnamo mwaka wa 2020, COVID-19 ilidororeshsha hali hiyo kwenye mambo kadha ikiwa ni pamoja na faragha, uhuru wa kujieleza mtandaoni, ufuatiliaji, utambulisho wa kidijitali, ufikiaji.***

14. Accelerating Digital Transformation in Rwanda,2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda
15. Electricity access, Rwanda Energy Group, https://www.reg.rw/what-we-do/access/
16. Rwanda Telecentre Network, 2020, https://rtn.rw/about/
17. Smart Rwanda Master Plan, 2015, https://www.minict.gov.rw/policies?tx_filelist_filelist%5B%40widget_0%5D%5BcurrentPage%5D=2&cHash=16083ab4b0499921686749e2c5213490
18. "Rwanda: Lockdown Arrests, Abuses Surge", "End media Crackdown, Mass Arbitrary Arrest", Human Rights Watch,24 April 2020, https://www.hrw.org/news/2020/04/24/rwanda-lockdown-arrests-abuses-surge
19. State of Internet Freedom in Rwanda, 2019,
20. "Man arrested for publishing rumours", The New Times, July 13,2020, https://www.newtimes.co.rw/news/covid-19-man-arrested-publishing-rumours
21. Law on prevention and punishment of cybercrimes, 2018, https://rura.rw/index.php?id=104&tx_news_pi1%5Bnews%5D=603&tx_news_pi1%5Bday%5D=27&tx_news_pi1%5Bmonth%5D=9&tx_news_pi1%5Byear%5D=2018&cHash=cf6a0de5282574dd3c3a8081a6348b83
22. Cabinet Communique, 2020,

ya YouTube, alikamatwa siku chache baada ya kutoa ripoti kuhusu madai ya ukiukwaji wa haki lawama ilielekezewa jeshi katika kitongoji cha Kigali. Kamati ya Kulinda Wanahabari ilitoa wito kwa mamlaka ya Rwanda kuwezesha waandishi wa habari na wafanyakazi wa vyombo vya habari kufanya kazi zao bila "kuingiliwa".[23]

Kwa kuongezea, vifungu vya makosa ya jinai katika Sheria ya Makosa na Adhabu ya Rwanda vimetumika kuwahukumu wataalam wa habari na wakosoaji.[24] Hata hivyo, mnamo 2018 na 2019 vifungu hivyo vilifutwa kutoka Kanuni ya adhabu.[25] Licha ya kufutwa kwa vifungu ambavyo vinaweza kutumiwa kuzuia uhuru wa kujieleza mtandaoni na nje ya mtandao, wengine bado wana wasiwasi na wanaamini kuna njia zingine za kuwanyamazisha wakosoaji. "Linapokuja kwa suala la nyanja za kisiasa na uhuru wa waandishi wa habari nchini Rwanda, utawala wa Kagame unaonekana kuwa kizingiti kwa maendeleo halisi. Kauli yake kuhusu kukashifu inaweza kusababisha kufutwa kwa sheria, lakini hilo halimfanyi kuwa mwenye maono ambaye anapaswa kukumbatiwa", aliandika Fred Muvunyi, mwandishi wa habari wa Rwanda, mwenyekiti wa zamani wa shirika la wanahabari nchini Rwanda linalojidhibiti lenyewe.[26] "Njia nyingine zipo za kuwatesa wakosoaji au kuwabana upinzani", aliongeza.

## FARAGHA NA UFUATILIAJI

Mnamo mwaka wa 2019, Rwanda iliridhia 'Mkataba wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulindaji wa Data za Kibinafsi'.[27] Baraza la mawaziri la Rwanda liliidhinisha rasimu ya sheria ya ulindaji wa data na faragha mnamo Oktoba. Madhumuni ya rasimu ya sheria hiyo ni kutoa utaratibu "utakaohakikisha" ulindaji na faragha ya data ya kibinafsi. Katika uhariri wenye mada, "Muda wa Ulindaji wa data umewadiwa, harakisheni" Gazeti la Rwanda Leo lilisema muswada huo ulikuwa umechelewa: "Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Wanyarwanda wanaofikia huduma za kidijitali, kutungwa kwa sheria hii kulikuwa kumechelewa sana. Mamilioni ya wanyarwanda tayari wanapata majukwaa ya kidijitali kwa mitandao ya kijamii, kusoma na kufanya kazi."[28] Walakini, rasimu ya sheria haiangazii maswala muhimu ya faragha yaliyoibuliwa kuhusu data ya kibinafsi kama vile utambulisho wa kidijitali na ,mengineyo.

Mnamo 2020, zana za ufuatiliaji zilitumika kuzuia kuenea kwa COVID-19, lakini ukosefu wa uwazi unaweza kuathiri haki za watu za faragha. Mnamo Julai, polisi ilifafanua kwamba utambulisho wa wanaokiuka kanuni za COVID-19 ungerekodiwa kwa njia ya kidijitali ili kuamua "hatua kali" iwapo visa vya kurudia ukiukaji vingejitokeza tena.[29]

> **"IMnamo 2020, zana za ufuatiliaji zilitumika kuzuia kuenea kwa COVID-19, lakini ukosefu wa uwazi unaweza kuathiri haki za watu za faragha."**

23. "Multiple Journalists arrested throughout covid-19 lockdown period", 9 September 2020,
24. CIPESA, State of Internet Freedom in Rwanda, 2019, https://www.opennetafrica.org/?wpfb_dl=103
25. "Rwanda court repeals law that bans satirical cartoons", Reuters, 24 April 2019, https://www.reuters.com/article/us-rwanda-politics-cartoons-idUSKCN1S02B0
26. "Opinion: Rwanda's Paul Kagame- an enemy of the media parading as a statesman", DW, 2 May 2019, https://www.dw.com/en/opinion-rwandas-paul-kagame-an-enemy-of-the-media-paradingas-a-statesman/a-48562042
27. "AU Convention is finally part of Rwandan Law", 2019, https://www.newtimes.co.rw/opinions/au-convention-finally-part-rwandan-law
28. "Editorial: Data Protection Law Long overdue, fast-track it", 11November 2020, https://rwandatoday.africa/rwanda/opinion/editorial-data-protection-law-long-overdue-fast-track-it-3018844
29. "Covid19:Police Outlines tough measures against errant violators"/, 24 July 2020, https://www.ktpress.rw/2020/07/covid-19-police-outlines-tough-measures-against-errant-violators/

Mnamo Mei, serikali ya Rwanda ilitumia zana za kidijitali kufuatilia visa vya maambukizi. Programu zilizotumia data za wasifu wa simu kuwafuatilia watu ambao walikuwa wakiwasiliana na wagonjwa wa COVID-19. Mfumo huo ungeweza kufuatilia na kuwafungia watu hao katika vituo vya kutengwa ili kuhakikisha kuwa hawatoki maeneo yao ya kutengewa.[30] WhatsApp binafsi, ujumbe wa Skype na barua pepe zimetumika kama ushahidi katika kesi za mahakama zinazoongeza wasiwasi kuhusu ukiukaji wa faragha na ufuatiliaji.[31] Uingiliaji wa mawasiliano kulitumika kukusanya ushahidi katika kesi ya Diane Rwigara, mkosoaji wa serikali, lakini upande wa mashtaka ulipoteza kesi hiyo mnamo 2018 kwa ukosefu wa ushahidi wa kutosha.[32]




> **“*WhatsApp binafsi, ujumbe wa Skype na barua pepe zimetumika kama ushahidi katika kesi za mahakama zinazoongeza wasiwasi kuhusu ukiukaji wa faragha na ufuatiliaji.*"**

## UFIKIAJI NA GHARAMA YA MTANDAO NA TEKNOLOJIA

Licha ya kuongezeka kwa upenyaji wa mtandao, wengi wanasalia kutengwa kwa sababu ya umaskini na kama matokeo, hawawezi kupata vifaa vya kidijitali, wanakosa uunganishwaji kwa mtandao, wakati wengine hawana ujuzi kidijitali. Bei ya wastani ya kila mwezi ya GB1 kila mwezi ilikuwa $ 0.56 ya Amerika mnamo 2018, sawa na 5.1% ya mapato ya wastani ya kila mwezi. Hii ni zaidi ya maradufu ya lengo la Alliance for Affordable Internet la 2% na inayofanya gharama kuwa ya juu kwa wengi.[33] Hivi sasa GB 1.5 ya 3G inagharimu wastani wa dola 2 za Marekani (USD) ambayo bado haiwezi kugharamiwa na wengi.[34] Pamoja na hayo, gharama ya mtandao nchini Rwanda inasemekana kuwa moja ya bei nafuu zaidi barani Afrika.[35] Wakati wa kufungiwa kipindi cha COVID-19, elimu ilikuwa moja ya maeneo yaliyoathiriwa na kutengwa kidijitali haswa kwa sababu ya ukosefu wa umudu. “Idadi kubwa ya wanafunzi au wazazi hawana kipakatalishi au simu za rununu, na wengi wao hawawezi kupata kazi ambazo waalimu wamekuwa wakituma kupitia vikundi vya WhatsApp tangu kufungiwa kipindi cha COVID-19,” alisema mkuu wa chuo.[36]Takwimu kutoka Benki ya Dunia zinaonyesha 37% haimiliki simu wakati wengi wanategemea huduma za 2G zilizo na vipengele vichache.[37]

30. “Rwanda opts for digital tools in COVID-19 contact tracing”, 2 May 2020, https://allafrica.com/stories/202005040293.html
31. State of Internet Freedom in Rwanda, 2019,
32. “Rwandan court acquits the Rwigaras”, 2018, https://www.theeastafrican.co.ke/news/ea/Rwandan-court-acquits-the-Rwigaras/4552908-4884232-ypfb4s/index.html
33. Accelerating Digital Transformation in Rwanda, 2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda
34. Airtel, Internet services bundles, https://airtel.co.rw/internetservice/databundle
35. “Rwandans spend 7% of their income on Internet”, 2020, https://www.newtimes.co.rw/news/report-rwandans-spend-7-their-income-internet
36. “Leading a school during covid-19 crisis: an interview with a school leader”, page 12, 21 September 2020, https://rwanda.vvob.org/news/online-and-distance-learning-educational-response-covid-19-crisis
37. Accelerating Digital Transformation in Rwanda, 2020, https://documents.worldbank.org/en/publication/documents-reports/documentdetail/912581580156139783/rwanda-economic-update-accelerating-digital-transformation-in-rwanda

## JINSIA NA UFIKIAJI

Usawa wa kijinsia umekuwa kwenye kitovu cha sera za Rwanda kuziba pengo la kidijitali. Programu kama vile 'Wasichana kwenye ushauri wa TEHAMA na mitandao', 'Balozi wa Kidijitali', 'Wanawake kwenye TECH' zina jukumu muhimu. Hata hivyo, wanawake bado wako nyuma katika TEHAMA. Takwimu zinaonyesha kuwa ufahamu wa kompyuta bado uko chini lakini uko chini zaidi miongoni mwa wanawake kuliko wanaume wenye umri kati ya miaka 15-30 (10.7% ikilinganishwa na 13.8%). Ongezeko tangu 2014 hadi 2018 limekuwa la chini sana. Mwelekeo huo umezingatiwa kwa wanawake na wanaume kati ya miaka 15-24 na kwa idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi.[38] Takwimu kutoka RURA zinaonyesha kuwa kufikia Juni 2020, 26% ya wafanyakazi wa mawasiliano, ambayo huajiri watu 1,127, ni wanawake wakati 74% ni wanaume.[39]

Kupanua upatikanaji wa vifaa vya kidijitali katika nyumba na shule zote; kuongeza muunganisho na kuboresha ufikiaji wa maudhui ya kidijitali ni baadhi ya suluhisho la pengo la kidijitali.[40] Wakati unapimwa dhidi ya Azimio kuhusu Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Upataji wa Habari barani Afrika,[41] wasiwasi unaongezeka haswa kwa kuhusu uhuru wa kujieleza. Huku kunathibitishwa haswa na kanuni kali za vyombo vya habari kama vile mchakato kuanzisha mashirika ya na vyombo vya habari na idhini.[42] Kuhusiana na haki ya kupata habari, Rwanda ilitunga sheria Nambari 04/2013 ya 08/02/2013 inayohusiana na upatikanaji wa habari,[43] ambayo licha ya kuwa sheria yenye manufaa, upatikanaji wa habari unabaki kuwa changamoto kwa sababu ya kukataliwa wa ombi la taarifa.[44]



38. National Gender Statistics Report, 2019, https://www.statistics.gov.rw/publication/national-gender-statistics-report-2019
39. Quarterly ICT statistics report, June 2020, https://rura.rw/fileadmin/Documents/ICT/statistics/Quarterly_ICT_Statistics_report_as_of_June_2020_.pdf
40. Online and distance learning: Education response to the COVID-19 crisis,21 September 2020, https://rwanda.vvob.org/news/online-and-distance-learning-educational-response-covid-19-crisis
41. Safeguarding Civil Society in East Africa, 2017, https://smallmedia.org.uk/work/safeguarding-civil-society-east-africa
42. Law relating to access to Information, 2013,
43. "Despite a Progressive law, Access to Information ", 2020, https://panafricanvisions.com/2020/11/despite-a-progressive-law-access-to-information-remains-a-challenge-in-rwanda-report/

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hali ya haki za kidijitali na ujumuishaji nchini Rwanda mnamo 2020 imeathiriwa pakubwa na janga la COVID-19 wakati wa kufungwa kwa nchi ikiwa ni pamoja na vizuizi vinginevyo vilivyofuatia. Hili limedhihirishwa kwenye mazoea ya ufuatiliaji uliyostahiki ambao haukuwa wa uwazi na kulileta hali ya wasiwasi kuhusu ukiukaji wa haki za faragha na za kidijitali kama ilivyoangaziwa katika ripoti nyingi zilizotajwa. Mazoea ya kale ambayo husababisha sheria za nchi na vifungu ambavyo vinaweza kuzuia uhuru wa kujieleza mtandaoni na nje ya mtandao viliendelezwa 2020. Licha ya kuongezeka kwa upenyaji wa mtandao, pengo la kidijitali linakua kwani wengi hawawezi kufikia na kutumia mtandao kwa sababu ya gharama za juu za huduma za mtandao na vifaa vya kidijitali, haswa simu za rununu. Takwimu zinaonyesha pengo la kijinsia la kidijitali linabaki kuwa changamoto muhimu licha ya nchi kuanzisha mipango ya kujumuisha wanawake katika sekta ya TEHAMA na kuwawezesha kushiriki katika mabadiliko makubwa ya kidijitali. Kwa kupanua ufikiaji wa vifaa vya kidijitali na huduma za mtandao kwa nyumba, hii inaweza kusaidia kupunguza mwanya wa kidijitali, haswa ikiwa itafanywa kwa kushirikiana na kampuni za mawasiliano, watoa huduma za kidijitali, vituo vya huduma za mtandao (telecentres) na wadau wengine wa TEHAMA Serikali inapaswa pia kuwekeza zaidi katika miundombinu ya kidijitali ili kukuza mazingira wezeshi kwa kuwachochea waendeshaji simu na wawekezaji wengine wa TEHAMA kuunganisha idadi ya watu wa vijijini. Kuenea kwa mtandao bila matumizi hakupunguzi mwanya wa kidijitali.

Licha ya kuondolewa kwa vifungu vya makosa ya jinai katika sheria ya adhabu; Kifungu kuhusu uchapishaji uvumi ambacho kiko katika sheria ya usalama wa mtandaoni hakiko bayana na kinapaswa kurekebishwa au kufutwa kwa sababu kinaweza kuzuia uhuru wa kujieleza mtandaoni.

Pengo la kidijitali la kijinsia linazuia mafanikio ya usawa wa kijinsia ya nchi, ambayo yanalenga kukuza ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanawake. Hili linapaswa kuimarishwa zaidi kwa matokeo bora na mamlaka inapaswa kuwasihi wanawake wengi kujiunga na sekta ya TEHAMA kwa kusisitiza kampuni za mawasiliano kuajiri wanawake zaidi na kujumuisha ukuzaji wa jinsia katika sera ya ajira.

Rasimu ya sheria iliyoidhinishwa ya ulindaji wa data inapaswa kuharahikishwa lakini ibadilishwe ili kujumuisha vifungu vingine vya ulindaji wa data ambavyo vinagusia utambulisho wa kidijitali na utumiaji wazi wa data ya kibinafsi na kampuni za kibinafsi na za umma.

# LONDA

**RWANDA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

PARADIGM INITIATIVE

**Paradigm Initiative**

374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria

Email: media@paradigmhq.org

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ